

# Loti na Familia Yake

MWANZO 19:1-26

Chagua mazoezi yanayofaa mahitaji na mapendezi ya mtoto wako. Fanyeni mazoezi hayo mkiwa familia.



## SOMA MWANZO 19:1-26

Kisha, soma hadithi ya Biblia iliyochorwa (kwenye intaneti au kwenye karatasi iliyochapishwa), na mzungumzie maswali mwishoni mwa somo.


**JARIBU KUFANYA HIVI:** Sikiliza drama ya Kiingereza kumhusu Loti na babu yake Noa, yenye kichwa “*Jehovah’s Judgment Against Law-Defying People*” (Hukumu ya Yehova Dhidi ya Watu Wanaokaidi Sheria). Pakua drama hii kwenye [www.jw.org/Publications/Dramas](http://www.jw.org/Publications/Dramas).

## MAZOEZI ZAJIDI UNAYOWEZA KUCHAPA



### MAZOEZI YA PICHA

**UNGANISHA NUKTA** Kwa ajili ya watoto wadogo (miaka 3 hadi 5): Waombe watoto waunganishe nukta, na wapake rangi picha. Waombe waeleze ni jambo gani linalotukia katika picha.



### MAZOEZI YA KUJIFUNZA

**NASABA** Kwa watoto wakubwa (6 hadi 10): Waombe wajaze majina ya mataifa yaliyotokana na uzao wa Loti na watu wake wa ukoo.



### KUSANYA NA UJIFUNZE

**KADI ZA WAHUSIKA KATIKA BIBLIA** Soma mambo machache kumhusu. Uliza maswali yaliyo kwenye kadi. Kwa kutumia chati zinazoonyesha miaka na matukio za kadi hiyo na kadi nyingine mlizo nazo, msaidie mtoto wako apace wahusika wa Biblia kulingana na wakati na matukio.